**336/1**
**LUGHA NA**
**FASIHI YA KISWAHILI**
**Paper 1**
2 hours

# Apex Examination Council

# PRE- MOCK EXAMINATIONS 2025

## Uganda Certificate of Education

**LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI**

**Karatasi ya Kwanza**

(Uandishi wa Insha na Ufupisho)

Saa mbili

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

Karatasi hii ina sehemu **mbili; A** na **B**. Ina maswali matatu.

Jibu maswali **mawili** kwa ujumla ukichagua **moja** kutoka kila sehemu.

Swali la ziada halitasahihishwa.

Majibu **yote** yaandiikwe kwenye kijitabu ulichopewa.

## SEHEMU A.

## UANDISHI WA INSHA

**Ama**

**1.** Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda nchi yake kutoka moyoni mwake. Uzalendo ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii/Nchi. Binadamu kuitwa mzalendo, anastahili kuonyesha vitendo vya uzalendo. Rafiki yako anasomea Vision Shule ya Upili wilayani Kisoro. Shuleni kwao, hawaelewi vizuri mambo ya uzalendo. Rafiki yako huyo anaitwa Rhoda. Mwandikie barua ukimwelezea juu ya suala hili. (Alama 33).

**Au**


**2**. Amani na usalama ni masuala muhimu yanayopachana. Masuala haya ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Katika nchi zenye amani na usalama Kuna mambo mbalimbali yanayotendeka/ yanayofanyika. Pia kuna mambo au vitendo kadhaa vinavyotendeka katika nchi ambazo hazina/ zinakosa amani na usalama. Nchini, Kuna mashirika tofauti ambayo hulinda na kuendeleza amani na usalama. Wewe umeombwa kutoa hotuba Kwa wanafunzi wenzako kuhusu masuala hayo juu. Andika hotuba utakayowasomea. (Alama 33).

Apex Examination

## SEHEMU B

## UFUPISHO

**3.** Soma mazungumzo yafuatayo na ujibu maswali.




**Waandamanaji:** *(Kunasikika makelele katika Barabara ya Bombo karibu na Chuo kikuu cha Makerere)* Haki zetu! Haki zetu! Tunataka haki zetu ziheshimiwe!

**Polisi:** Ondoka hapa mara moja! Sitaki kusikia kelele!

**Waandamanaji:** Hatutoki hapa! Tumechoshwa nanyi polisi ambao hamjui Haki za raia.

**Polisi:** Maana ya haki si kusumbua utaratibu!

**Waandamanaji:** *(Wanaendelea na kelele).* Tunataka kujua kwa nini kodi imepandishwa?

**Polisi:** Toka hapa nenda bungeni mahali pa wanasiasa.

**Waandamanaji:** Tuna haki yetu ya kufanya maandamano popote pale almuradi hatujavunja sheria.

**Polisi:** Mtaondoka au tutawafyatulia risasi?

**Waandamanaji:** Hatuondoki! Fyatua, hata ukituua hatujali, tunataka serikali ituelezee kwa nini kodi inapandishwa kiholela.

**Polisi:** (Askari mmoja anafyatua risasi na kujeruhi mmoja wa waandamanaji)

**Waandamanaji:** (Waandamanaji wanamrukia askari huyo aliyefyatua) Kwa nini umemwua mwenzetu? Na wewe utakufa. *(Wanamfukuza Polisi)*

**Polisi:** (Anajaribu kukimbia kusogelea askari wenzake, lakini wapi)

**Waandamanaji:** (Wanamzingira Polisi. Wanampiga na kumwua)

**Maswali:**

(a) Ni nani wanaozungumza? (Alama 02)

(b) Wanazungumza wakiwa wapi? (Alama 02)

(c) Andika kichwa kinachofaa mazungumzo haya. (Alama 02)

(d) Je, ni haki ipi ambayo waandamanaji walikuwa wanadai? (Alama 02)

(e) Kwa nini polisi walikataa kuwakubali kufanya maandamano? (Alama 02)

(f) Askari polisi hatimaye alikiuka haki ipi? (Alama 02)

(g) Tunastahili kufanya maandamano kwa njia gani? (Alama 02)

(h) Ingawa waandamanaji walikuwa wanadai haki zao, ni haki gani ambayo mwishowe walikiuka? (Alama 02)

(i) Kama wewe ungekuwa jaji, waandamanaji ungewahukumu kwa kesi gani? (Alama 04)